

Maswali

1. Dorkasi aliishi wapi?
2. Dorkasi alitaka kufanya nini?
3. Dorkasi alikuwa mzuri kwa kufanya nini?
4. Dorkasi alishona nini?
5. Aliwapa wakina nani hizo nguo?
6. Nini ilifanyika wakati Dorkasi alikuwa mgonjwa sana?
7. Wanafunzi walienda kuleta nani?
8. Petro alifanya nini?
9. Mungu alijibu maombi ya Petro namna gani?
10. Watu wa Yafa walifanya nini waliposikia kwamba Petro alikuwa amemfanya Dorkasi kuwa hai tena?

Majibu

1. Dorkasi aliishi Yafa.
2. Dorkasi alitaka kusaidia watu.
3. Dorkasi alikuwa mzuri kwa kushona.
4. Dorkasi alishona nguo nyingi.
5. Alipea watu maskini hizo nguo.
6. Dorkasi alikufa.
7. Wanafunzi walileta Petro.
8. Petro aliomba Mungu.
9. Mungu alimfanya Dorkasi kuwa hai tena.
10. Watu wa Yafa waliamini kwa Yesu.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



47 Dorkasi

Marejeo

Matendo ya Mitume 9: 36 – 42

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba tunaweza kutumia vibawa vyenye Mungu ametupa kusaidia wengine

Maneno maalum

- 47.1 Yafa + Dorkasi + saidia watu + watu maskini + kushona + tengeneza nguo.
- 47.2 Dorkasi + mgonjwa sana + alikufa + wanafunzi + mlete Petro
- 47.3 Petro + omba + Dorkasi, amka + Mungu alijibu + Dorkasi aliamka + kila mtu alifurahi
- 47.4 Watu wa Yafa + sikia + Dorkasi yu hai tena + amini

47.1 Yafa ulikuwa mji mzee kando ya bahari. Katika mji huu, aliishi mwanamke mungwana, aliyeitwa Dorkasi. (Dorcasi alikuwa na jina lingine. Wakati mwingine aliitwa Tabitha). Dorkasi alijua ni vitu gani vya ukarimu vyenye Yesu alitaka tufanye kusaidia wenzetu. Alijua kwamba wanafunzi na marafiki wao wanatakiwa nao wajaribu kusaidia watu. Dorkasi naye alitaka kusaidia.

Kwa mji wa Yafa kulikuwa na watu wengi maskini wenye nguo zao zilikuwa zimeraruka na zingine kuuu. Dorkasi alikuwa mzuri kwa kushona, kwa hivyo alifikiria na akapanga njia ya kusaidia watu. Alinunua vifaa na akachukua muda mrefu akishona nguo. Dorkasi alishona nguo kwa bidii. Alipomaliza kushona, aliwapa watu waliokuwa maskini kwa huo mji. Wakati wote Dorkasi alishughulika na kushona nguo. Alishonea watu wengi sana waliokuwa maskini wa nguo.

47.2 Lakini siku moja Dorkasi alikuwa mgonjwa. Hakuweza kushona siku hiyo. Muda si muda, Dorkasi alilala kitandani. Alikuwa mgonjwa sana. Marafiki wake walikuja kumhudumia kwa sababu alikuwa mkarimu sana. Mwaishowe Dorkasi alikufa, na marafiki wake walihuzunika sana.

Baadhi ya wanafunzi walisikia kwamba Petro alikuwa anaishi kwa mji karibu. Labda anaweza kusaidia. Watu wawili walitumwa kwa Petro. Walimuuliza, “Tafadhali kuja na sisi mpaka Yafa.” Petro aliondoka nao. Petro alipofika Yafa, walimpeleka kwa orofa penye Dorkasi alikuwa amekufia.

47.3 Petro alijua kwamba Mungu ndiye hupeana uhai. Alitaka awe peke yake na Mungu. Kwa hivyo aliuliza kila mtu atoke chumbani. Halafu alipiga magoti na kuomba Mungu. Aliuliza Mungu amrudishie Dorkasi uhai. Aliambia aliyekufa, “Dorkasi, amka.”

Mungu alijibu maombi ya Petro. Dorkasi alifunguo macho na akaamka. Petro alimzaidia kukaa. Dorkasi alikuwa hai na mzima tena! Petro aliwaita wanafunzi na marafiki wa Dorkasi. Walikuwa na furaha iliyoje walipomwona rafiki wao mkarimu akiwa hai tena!

47.4 Watu wote wa Yafa walisikia kwamba Dorkasi alikuwa amekufa na Petro akamfanya akawa hai tena. Lilikuwa jambo la ajabuje! Kwa hivyo watu wa Yafa waliamini kwa Yesu.

